JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 007 JULAI, 2021

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

1 NAIBU SPIKA: VYOMBO VYA HABARI TENGENI MUDA WA KUTOSHA KURUSHA TAARIFA ZA HALI YA HEWA

2 MAWAZIRI SADC WAPITISHA MAAMUZI KUMI YA SEKTA YA HALI YA HEWA

3 FAHAMU ZAIDI: MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTABIRI WA HALI MBAYA YA HEWA

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

JARIDA LA MWEZI

02 TOLEO NA. 007 JULAI, 2021

TMA TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

KITAIFA

NAIBU SPIKA: VYOMBO VYA HABARI TENGENI MUDA WA KUTOSHA KURUSHA TAARIFA ZA HALI YA HEWA

Dar es Salaam

Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania Mhe. Dkt. Tulia Ackson akipata maelezo ya namna taarifa za hali ya hewa za muda mrefu zinavyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya sekta mbalimbali ikiwemo miradi ya kimkakati kutoka kwa Meneja wa Klimatolojia, TMA, Dkt. Hashim Ng'ongolo wakati alipotembelea ofisi za TMA, Makao Makuu, Ubungo Plaza, Dar es Salaam, Tarehe 09/07/2021.

Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson (MB) ametoa wito kwa vyombo vya habari kutenga muda wa kutosha wa kurusha taarifa za hali ya hewa mara kwa mara ili kusaidia wananchi kuzipata kwa wakati na kuzitumia kwa ufanisi zaidi. Aidha, alieleza kuwa kutokana na muda wa habari ya hali ya hewa kuwa mfupi, taarifa zinatolewa kwa ujumla na kwa ufupi, kitu ambacho kinaweza kuathiri matumizi yake.

"Nitoe wito kwa vyombo vya habari kuangalia namna ambavyo watakuwa wanazitumia taarifa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kuzitoa mara kwa mara ili kutusaidia sisi wananchi kujiandaa nakufanya maamuzi sahihi katika mipango yetu, tuangalie kama vyombo vingine vya habari vya mataifa ya nje, ukifungua kila wakati unaangalia hali ya hewa"Alisema Dkt. Tulia wakati alipotembelea Makao Makuu ya TMA.

JARIDA LA MWEZI

03 TOLEO NA. 007 JULAII, 2021

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

Aliendelea kusema kuwa, alichojifunza katika ziara yake fupi katika ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, ni kuwa taarifa zipo, lakini kwa ajili ya muda mfupi basi Mamlaka inalazimika kuziweka katika huo muda mfupi. Kwa upande mwingine, alito wito kwa wananchi kuitembelea Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ili kujifunza masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na namna taarifa za hali ya hewa zinavyochakatwa kitaalamu hadi kumfikia mtumiaji.

Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania Mhe. Dkt. Tulia Ackson akijionea hindi utabiri wa hali ua hewa kila siku unavyorekodiwa katika studio za TMA kwa ajili ya kuruka katika vyombo mbalimbali vya habari nchini wakati alipotembelea ofisi za TMA, Kituo Kikuu cha Utabiri, Ubungo Plaza, Dar es Salaam, Tarehe 09/07/2021.

JARIDA LA MWEZI

04 TOLEO NA. 007 JULAI, 2021

TMA TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

KIMATAIFA

MAWAZIRI SADC WAPITISHA MAAMUZI KUMI YA SEKTA YA HALI YA HEWA

Dar es Salaam

Tanzania imeshiriki katika mkutano wa Mawaziri wa SADC wenye dhamana na masuala ya Uchukuzi, TEHAMA, Habari na Hali ya Hewa (Meeting of SADC Ministers responsible for Transport, ICT, Information and Meteorology), uliofanyika kwa njia ya mtandao kuanzia tarehe 6 hadi 9 Julai, 2021 nakufanikiwa kupitisha maamuzi kumi ya sekta ya hali ya hewa.

Katika mkutano huo, kiongozi wa mkutano ngazi ya Mawaziri kwa Tanzania alikuwa ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Dkt. Mhandisi Leonard Chamuriho (Mb), akisaidiana na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb), na kujumuisha wataalamu kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi.

Miongoni mwa maamuzi yaliyopitishwa ni pamoja na hadidu za rejea za kufanya mapitio ya Itifaki ya SADC ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa kwa lengo la kuiboresha zaidi ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa ya huduma

JARIDA LA MWEZI

05 TOLEO NA. 007 JULAI, 2021

TMA TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

za hali ya hewa katika kanda ya SADC. Aidha, masuala mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na kuoanisha sera za wadau wa huduma za hali ya hewa katika kanda ya SADC na hitaji la taasisi zote za hali ya hewa katika nchi za SADC kupata vyeti vya kimataifa vya ubora katika utoaji wa huduma za hali ya hewa vya ISO 9001:2015, ambapo TMA wamekwisha pata cheti hicho.

Katika hatua nyingine, mkutano huo ulipitisha mpango wa kuhuisha shughuli za Umoja wa Taasisi za Hali ya Hewa SADC (MASA Rescue Plan). Vilevile, Mkutano uliziomba Nchi Wanachama kujitolea kuwa Mwenyeji wa Sekretarieti ya MASA, ambapo Tanzania ambaye kwa sasa ndiye Mwenyekiti wa MASA kupitia TMA, iliwasilisha nia ya kuwa mwenyeji wa sekretarieti ya MASA baada ya kipindi cha mpito cha mwaka mmoja kukamilika mwezi Machi, 2022.

METEOROLOGICAL ASSOCIATION OF SOUTHERN AFRICA
WEATHER CLIMATE WATER

Mkutano huo wa SADC ulifanyika katika hatua mbili, ambapo ulianza katika ngazi ya Makatibu Wakuu kuanzia tarehe 6 hadi 8 na kufuatiwa na ngazi ya Mawaziri tarehe 9 Julai, 2021. Mkutano huo ulifanyika chini ya ya uenyekiti wa Nchi ya Msumbiji ambapo ulijadili utekelezaji wa maamuzi ya mkutano wa Mawaziri uliofanyika mwaka 2019 jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dkt. Agnes Kijazi, akiongoza mkutano huo wa SADC ngazi ya wataalamu wa Hali ya Hewa tarehe 8 Julai,

Mawaziri wa SADC wenye dhamana na masuala ya sekta za Uchukuzi TEHAMA, Habari na Hali ya Hewa hukutana kila mwaka kama ilivyo kwa sekta zingine kujadili utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya kisekta katika eneo la SADC na kutolea maamuzi mapendekezo ya wataalamu katika sekta husika.

JARIDA LA MWEZI

06 TOLEO NA. 007 JULAI, 2021

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

FAHAMU ZAIDI:

MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTABIRI WA HALI MBAYA YA HEWA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI.
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Fomu Na. 722E_3 (Rev.02/2020)

Matarajio ya Hali Mbaya ya Hewa kwa siku Tano

Yametolewa Leo Jumamosi: Tarehe 24-07-2021, Saa 9:30 mchana

Jumamosi: 24-07-2021

TAHADHARI ya upepo mkali unaofikia kilomita 50 kwa saa na mawimbi makubwa yanayofikia mita 3.0 imetolewa kwa baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi (mikoa ya Lindi, Mtwara, Tanga, Dar es Salaam na Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia) pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na ziwa Victoria (mikoa ya Mwanza, Geita, Kagera, Simiyu na Mara).
UWEZEKANO WA KUTOKEA: MKUBWA.
KIWANGO CHA ATHARI ZINAZOWEZA KUTOKEA: WASTANI.

ANGALIZO la upepo mkali unaofikia kilomita 40 kwa saa limetolewa kwa baadhi ya maeneo ya ziwa Nyasa (mikoa ya Ruvuma Njombe na Mbeya) na ziwa Tanganyika (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa)
UWEZEKANO WA KUTOKEA: WASTANI.
KIWANGO CHA ATHARI ZINAZOWEZA KUTOKEA: WASTANI.
UWEZEKANO WA KUTOKEA: WASTANI.
KIWANGO CHA ATHARI ZINAZOWEZA KUTOKEA: KUBWA.

Athari zinazoweza kujitokeza
Kuathirika kwa baadhi ya shughuli za usafirishaji na uvuvi, Kuanguka kwa miti midogo, nyumba zenye mapaa yasiyoimara kuezuliwa, vumbi kupeperushwa na kupunguza uono na kuharibika kwa mazao katika maeneo machache.
Tafadhali chukua hatua.

Je ukiona rangi hizi kwenye utabiri wa matarajio ya hali mbaya ya hewa inamaanisha nini?

ALAMA	MAELEZO
	ANGALIZO ◆ Rangi ya njano inawakilisha angalizo dogo linalotolewa kuashiria uwezekano wa kutokea kwa hali mbaya ya hewa yenye athari.
	TAHADHARI ◆ Rangi ya chungwa inawakilisha tahadhari kubwa inayotolewa kuashiria uwezekano wa kutokea kwa hali mbaya ya hewa yenye athari.
	TAHADHARI KUBWA ◆ Rangi ya nyekundu inawakilisha tahadhari kubwa sana inayotolewa kuashiria uwezekano wa kutokea kwa hali mbaya ya hewa yenye athari.

JARIDA LA MWEZI
07 TOLEO NA. 007 JULAI, 2021
TMA TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

KISWAHILI CHETU

ISTILAHI ZA HALI YA HEWA

Tuangazie herufi E:

glaciations	mto barafu
glacier`	barafuto
green house effect	athari za gesi hamijoto
green house gasses	gesi hamijoto

Barafuto iliyopo mlima wa Kilimanjaro - Tanzania

JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:

Mhariri
Monica Mutoni

Waandishi
Monica Mutoni
Wilbert Muruke

Msanifu Kurasa
Kennedy Mgeta

Shukrani
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa
Kituo Kikuu cha Utabiri

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

tanzaniametagency

TMAonline TV

Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
388 Br. Morogoro
S.L.P 3056,
16102 Dar es Salaam, Tanzania.